www.ippmedia.com

Alasiri Online

Alhamisi Februari 21, 2019 Tanzani 500/- Kenya 50/-



# MOBETTO ATIMKA

## OMMY DIMPOZ, ALI KIBA VS DIAMOND, HARMONIZE



# MOBETTO ATIMKA

Na Mary Kadoke

MAPENZI ya ulaghai yamchosha mwanamitindo maarufu nchini, Hamisa Mobetto na kuamua kushika hamsini zake baada ya kupenda pasipopendeka.

Amedhihirisha hayo kupitia ngoma yake mpya inayowika mjini kwa sasa 'Sawa' baada ya kutamba na kibao cha Tunaendanana hapo awali.

Akizungumza na Alasiri Online Hamisa amesema lengo la kazi hii ni kukazia suala la kuthaminiana hasa kwa wapenzi.

Akiongeza kuwa mwisho wa dharau na manyanyaso katika mahusiano ni majuto na kwa wakati huo mtendwa anakuwa kashafungasha virago vyake na pengine kumpata yule anayetuliza moyo wake.

"Si kila mara mwanaume au mwanamke atavumilia visa vya hapa na pale anavyofanyiwa na mpenzi wake, kuna muda inafika mtu anasema basi sawa acha maisha yaendelee," amesema.

"Unafanya kila kitu ili mwenzako afurahi, lakini unachopanda mavuno yanakuwa kupigwa na kutukanwa, sasa mwingine anaona haya ya nini bora kuachana," amesema.

Kazi hii kwa upande wa sauti imepikwa na mtayarishaji Bob Maneck na kuandikwa na Kusah.

Hii inakuwa ni kazi ya tatu tangu aachie kazi yake ya mwanzo ya Madam Hero, ikafuatiwa naTunaendana.

Mpaka sasa kazi hii mpya inaendelea kupata watazamaji katika mtandao wa YouTube ambapo mpaka sasa ina watazamaji 24,000.

# Barnaba- Hesima mbele



Na Anaeli Mbise

NYOTA wa muziki wa kizazi kipya Barnaba, amesema heshima kwa kila mtu imemfanya kutowapoteza mashabiki wake.

Akizungumza na Alasiri Online, Barnaba amesema kuwa sababu kubwa ya mashabiki kumkubali ni kutokana na misingi ya nidhamu aliyojijengea kwa watu.

"Sijisifii, lakini katika maisha yangu siwezi kumdharau mtu wala kumtukana, hilo limenifanya niwe mtu wa watu katika shughuli zangu za muziki," amesema Barnaba.

Msanii huyo amesema hata anapoitwa na watangazaji kwa ajili ya kufanya mahojiano katika redio au televisheni huwa anafika kwa wakati.

Kwa sasa anatamba na ngoma mpya inayokwenda kwa jina la Washa na ambayo pia inafanya vizuri katika vituo vya redio na televisheni.

# HAMASA YA KUOA HIYO!!!



Na Anaeli Mbise

MWANAMUZIKI wa Hip-hop Darassa ametoa ngoma mpya, inayokwenda kwa jina la Chanda Chema ambayo ameshirikisha Marioo.

Akizungumza na Alasiri Online, mwanamuziki huyo amesema kuwa sababu za kutoa ngoma hiyo ni kwa ajili ya kuwaasa vijana ambao hawajao kufanya hivyo kwa maana bado mabinti wazuri na wenye tabia njema wapo na siyo vyema kuendelea na maisha ya 'ubachela'

"Nimeutunga kuhamasisha vijana kuwa walimbwende na wenye tabia nzuri za kuvutia ambao wanatamani pia ndoa ni wakuvalishwa pete na kuolewa kama wake kabisa," amesema Darassa.

Aidha mwanamuziki Marioo amesema ameshirikiana na Darassa kutokana na ngoma hiyo kuwa na maudhui ya kufanya vijana hasa wa kiume kutafakari namna ya kuoa wake sahihi.

Ngoma hiyo imetengenezwa na kuongozwa na Hanscana, huku video ikifanyika katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam.

## KAZINJA NA LADHA MPYA YA PRESHA

Na Anaeli Mbise

MUIMBAJI mpya wa nyimbo za Injili Christine Kazinja, amesema wimbo wake uitwao Kwa Yesu Hakuna Presha umefanya kuwa na faraja katika maisha yake.


Akizungumza na Alasiri Online, Muimbaji huyo ambaye awali alikuwa akiitwa Hafsa Kazinja, amesema aliandaa nyimbo saba mpya za Injili, lakini amelazimika kuongezea huo wa nane baada ya kuombwa na mashabiki wake.

"Ile sauti nilioimba katika wimbo wa 'Presha' wakati huo sijaokoka ndio nimeitumia katika huu mpya uitwao 'Kwa Yesu Hakuna Presha' umetokea kupendwa sana," amesema Kazinja.

Aidha, Kazinja ameongeza kuwa kufanya muziki wa Injili ni kutokana na kutokufanya vizuri katika tasnia ya Bongo fleva.

Mwaka 2006, Kazinja alitamba na wimbo wa Pressure ambao alimshirikisha Banana Zorro na kwa sasa ameamua kujikita katika Injili.





# Wema atoka korokoroni

**Na Mary Kadoke**

WEMA Sepetu ameahidi kubadilisha mwenendo wake hususani katika matumizi ya mitandao, baada ya Bodi ya Filamu Tanzania kumfungulia kuendelea na uigizaji.

Akifanya mahojiano na Alasiri Online ameishukuru bodi kwa kuthibitisha ubora wa nidhamu yake tangu afungiwe na kuahidi kumleta Wema mpya. "Naishukuru bodi ya filamu kunipa second chance baada ya kuithibitishia kwamba naweza kubadilika," amesema. "Nimejifunza kutokana na makosa na ninaahidi nitabadilisha mwenendo wangu cause nadhani kila mtu anajua jinsi gani ninavyoihusudu kazi yangu," amesema.

"Hivyo watu wategemee vitu vingi vizuri zaidi kutoka kwangu na ninawaahidi Watanzania kwamba sitawaangusha,"ameongeza.

Muigizaji huyu aliyewahi kutamba na filamu ya Family Tears alifungiwa na bodi hiyo kwa muda usiojulikana baada ya kutuma picha na video katika ukurasa wake wa Instagram @ wemasepetu zilizokuwa na maudhui ya ngono. Hivi karibuni bodi hiyo ilitangaza rasmi kuwa Wema alikuwa huru kufanya kazi zake za sanaa baada ya kuridhishwa na mwenendo wake. Alifungiwa Oktoba 29 mwaka jana na katibu wa bodi hiyo, Joyce Fisso.

Hapo awali akifanya mahojiano na Alasiri Online Fisso, alieleza sababu za kutoa kifungo hicho.

"Sisi kama bodi tunamhitaji katika tasnia hii kutokana na umahiri wake wa kazi ndani na nje ya nchi, hivyo kama bodi tuliamua kumfungia Wema kwa muda usiojulikana baada ya picha zake zenye maudhui ya ngono kutapakaa mitandaoni kinyume na taratibu tulizokubaliana," alisema.

Aidha, katibu huyo alidai kuwa mara kwa mara wamekuwa na warsha za kuwaelimisha na kushauriana na wasanii namna ya kutengeneza kazi bora na zilizo na viwango akitoa mfano wa mikoa ya Arusha, Songwe, Shinyanga na Mwanza ambayo wametoa mafunzo hayo.

# Ommy Dimpoz, Ali Kiba vs Diamond, Harmonize



**Na Anaeli Mbise**

KAMA wewe ni shabiki au mdau wa muziki wa Bongo fleva, basi mwaka huu kaa mkao wa kupata kolabo mbili matata.

Kolabo ya kwanza ni ya Ommy Dimpoz na Ali Kiba, ambayo itatoka mwezi mmoja baadaye. Akizungumza na Alasiri Online, Kiba amesema kuwa ameamua kufanya kolabo na Dimpoz baada ya kuugua kwa muda mrefu hospitalini.

"Ommy ni mmoja wa members wangu katika Rockstar na amepona tumeona ametoa ngoma mpya na kwa sasa tutatoa mpya ambayo naamini itakuwa kali," amesema Kiba. Kolabo nyingine kubwa inayosubiriwa kwa hamu ni ya Diamond Platnumz na Harmonize.

Hii inakuwa ni kolabo ya tatu kwa wasanii hao kutoka WCB, baada ya kufanya vizuri na zingine mbili za Bado na Kwangwaru.

Harmonize amesema kuwa ngoma hiyo mpya maandalizi ya kushoot video yameshakamilika na muda siyo mrefu itatoka.